

## Maswali

1. Waisraeli waliabudia Mungu wapi?
2. Meza iliyopembwa vizuri kwa fito iliitwaje?
3. Mbona Daudi alitaka kumjengea Mungu nyumba?
4. Mbona Daudi hakukubaliwa kumjengea Mungu nyumba?
5. Badala yake nani angejenga?
6. Daudi alitayarisha nini kujengea?
7. Baada ya Daudi kufa nani alikuwa mfalme?
8. Nani alimsaidia miti?
9. Hekalu ilijengwa wapi?
10. Ilionekana namna gani?
11. Nini iliwekwa ndani?
12. Mungu alionyeshaje kwamba atakuwa akikutana na watu huko?

## Majibu

1. Kwa hema.
2. Sanduku la agano.
3. Kwa sababu alikuwa na nyumba nzuri ya kifalme.
4. Kwa sababu alikuwa ni mtu wa vita na aliwauuwa watu wengi.
5. Sulemani mwanawe, mtu mwenye amani.
6. Alitengeneza ramani na kumsanyia vitu vyote vitakavyo tumiwa.
7. Sulemani mwanawe.
8. Hiram, mfalme wa Tiro.
9. Yerusalemu.
10. Ilikuwa na nguo nzuri na dhahabu na fedha nyingi.
11. Vyombo vya mbao, mshumaa, madhabahu na sanduku.
12. Aliijaza na Utukufu wake.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 15 Kujenga Hekalu

## Marejeo

1 Wafalme 6—8

## Kiini cha somo


Kuonyesha kwamba Mungu alitaka Sulemani amjengee Hekalu  
(*na so that He could meet with the Israelites there*)

(*English missing from book*)

## Maneno maalum

1. Abudu + hema + sanduku.
2. Daudi + Nyumba ya Kifalme + Nathani + jenga + hekalu.
3. Vita + ua + Sulemani + amani.
4. Daudi + tayarisha + kusanya + vifaa.
5. Daudi akafa + Hiram + Sulemani anza.
6. Jengo nzuri + dhahabu, fedha + vyombo + kimara cha mshumaa + madhabahu + sanduku.
7. Karamu + leta sanduku ndani + utukufu wa Mungu.

**15.1** Kwa mda mrefu Waisraeli walimuabudu Mungu katika hema. Walikutana naye mbele ya sanduku la maagano. Hii ilikuwa meza iliyopambwa vizuri na ilijengwa kwa fito. Watu walipokuwa wamekaa pahali pamoja, sanduku liliwekwa hemani.




**15.2** Daudi aliishi kwa nyumba nzuri ya kifalme. Alitaka amjengee pia Mungu nyumba nzuri. Akamwambia nabii Nathani alilonuia kulifanya. Lakini Mungu akamjia Nathani kwa ndoto na kumwambia, “Daudi asinijengee nyumba.”

**15.3** Daudi alikuwa amepigana vita vingi na kuwaua watu wengi. Nyumba ya Mungu anatakiwa iwe ya amani. Mungu alimwambia Daudi kwamba atakuwa na mwana atakayeitwa Sulemani. Sulemani atakuwa mtu wa amani, “Huyu atanijengea nyumba.”

**15.4** Bado Daudi alitaka kujengea Mungu nyumba ya kipekee. Akatengenezea Sulemani ramani ya kutumia. Akakusanya vifaa vingi vya hekalu. Akatafuta wajenzi wazuri. Akaambia viongozi wa Israeli kusaidia Sulemani. Alitaka hekalu ya Mungu iwe nzuri.

**15.5** Baada ya Daudi kukufa, Sulemani akawa mfalme. Hiramu mfalme wa Tiro alikubali kusaidia Sulemani ajenga hekalu. Hiramu alimpa Sulemani miti ya mierezi mingi. Walikuwa marafiki sana.



**15.6** Hekalu ilijengwa Yerusalemu. Ilikuwa kubwa na ya kifahari. Iitengenezwa na mawe mazuri na miti ya nguvu. Kila kitu kikafunikwa kwa dhahabu, au fedha au shaba. Kulikuwa na nguo nzuri. Hata vyombo vyote vilikuwa vizuri. Mishumaa iliwaka wakati wote kupeana mwangaza. Kulikuwa na madhabahu ya kutolea Mungu dhabihu. Kulikuwa na meza ya kipekee ya mkate wa kuhani. Pia kulikuwa na pahali pa kipekee pa sanduku la agano

**15.7** Kulifanywa karamu kubwa baada ya kumaliza kujenga hekuli. Sanduku la agano liliwekwa hekaluni. Mungu alijaza jekalu na utukufu wake. Mungu alianza kukutana na Waisraeli kwa hekalu.

